



# MRADI WA EAF-NANSEN

## Meneja/Afisa Uvuvi na Usimamizi wa Uvuvi unaojumuisha Ikolojia na Mazingira

Usimamizi wa Uvuvi unaojumuisha Ikolojia na Mazingira (Ecosystem Approach to Fisheries -EAF) unasisitiza juu ya hitaji la kuendeleza uimara wa ki-ikolojia kwa ajili ya uvuvi endelevu.

Lengo kuu la Usimamizi huu ni kupanga, kuendeleza na kusimamia uvuvi katika mwenendo unaoakisi mahitaji na shauku ya jamii bila kuharibu mbadala wa vizazi vijavyo kufaidika kutokana na uzuri wa huduma zitakazopatikana kutokana na kuhifadhi mfumo huu.

Utekelezaji wa Usimamizi wa Uvuvi unaojumuisha Ikolojia na Mazingira huweza kufaidisha Wavuvi, Jamii ya Wavuvi, Samaki na nchi kwa:

- kusaidia kufikia lengo la Millenia katika kuimarisha Usalama wa Chakula;
- kuimarisha juhudi za kitaifa na kimataifa za kupambana na umasikini;
- kuboresha maarifa juu ya rasilimali za uvuvi na kurudisha uwingi wa samaki;
- kuboresha ufuatiliaji wa uwingi wa samaki na mipango ya usimamizi wake;
- kuhimiza ushiriki wa wadau katika maamuzi ili kuwa na uhakika wa kutekeleza maamuzi hayo;
- kuweka sheria kwenye shughuli zenye madhara makubwa kwenye uvuvi.

Kwa maelezo zaidi kuhusu Usimamizi wa Uvuvi unaojumuisha Ikolojia na Mazingira Wasiliana na:

Mkurugenzi,  
Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi,  
Idara ya Maendeleo ya Uvuvi,  
Kitengo cha Uendelezaji wa Rasilimali za Uvuvi,  
S.L.P 2462,  
DAR ES SALAAM  
[www.eaf-nansen.org](http://www.eaf-nansen.org)



NANSEN PROJECT

Kusaidia nchi zinazoendelea kutekeleza Usimamizi wa Uvuvi unaojumuisha Ikolojia na Mazingira



# Wadau wa Uvuvi na Usimamizi wa Uvuvi unaojumuisha Ikolojia na Mazingira

Usimamizi wa Uvuvi unaojumuisha Ikolojia na Mazingira (EAF) huwa na faida kwa Samaki, Wavuvi, na Jamii za Wavuvi.

Usimamizi wa Uvuvi unaojumuisha Ikolojia na Mazingira unatambua kwamba usimamizi wa uvuvi ni muhimu ukazingatia Uwiano wa kibinadamu na Mfumo wa Ikolojia. Aidha, usimamizi wa aina hii huzingatia vipaumbele na matarajio ya jamii kwa wakati uliopo na ujao. Usimamizi huu unahakikisha kwamba maafisa uvuvi na wadau wengine wanakuwa na uono wa pamoja katika masuala yanayohusu uvuvi na rasilimali za zake.

Ushiriki wa wadau kama wavuvi, jamii ya wavuvi na wajasiriamali wa uvuvi katika usimamizi wa uvuvi na rasilimali zake ni muhimu ili kufanikisha utekelezaji wa malengo ya Usimamizi wa Uvuvi unaojumuisha Ikolojia na Mazingira. Faida ya kuwa na wadau kama hawa katika Usimamizi wa Uvuvi unaojumuisha Ikolojia na Mazingira ni pamoja na:

- kuchangia maarifa juu ya idadi ya samaki na maafisa uvuvi (Wanasayansi);
- kupokea na kutumia njia sahihi za uvuvi;
- kusaidia kutokomeza uvuvi haramu;
- kutambua umuhimu wa aina zote za samaki katika Bahari na kuhakikisha kuwa kiwango na idadi ya samaki wanaotakiwa kuvuliwa inazingatiwa;
- kusaidia kuanisha mfumo wa ki - ikolojia kwa kuepuka uvuvi usiotarajiwa (bycatch) kama ndege bahari (Seabirds), kasa, papa na aina nyingine ya viumbe walio katika hatari ya kutoweka;
- kushiriki katika zoezi la kutafuta ushauri wa kitaalam na mpango unaofanywa na mameneja/maafisa wa uvuvi.

Kwa kuzingatia Usimamizi wa Uvuvi unaojumuisha Ikolojia na Mazingira, Serikali inaweza kuendeleza na kuimarisha Sera, Sheria na Kanuni zilizopo ili kuhakikisha kwamba kunakuwa na uvuvi endelevu ili kutokomeza umasikini, kuongeza kipato na usalama wa chakula.



**NANSEN PROJECT**

Kusaidia nchi zinazoendelea kutekeleza Usimamizi wa Uvuvi unaojumuisha Ikolojia na Mazingira